BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MAENDELEO YA WANAWAKE, HABARI NA UTALII KUHUSIANA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA HABARI, UTALII NA MAMBO YA KALE KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambae ametuwezesha sisi kukutana hapa katika Baraza lako tukufu tukiwa katika hali ya uzima na afya njema.

Aidha Kamati ya Maendeleo ya Wanawake Habari na Utalii, inawapongeza Waislamu na wananchi wote nchini, na ulimwenguni kwa ujumla kwa kuidiriki tena Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, na hivi sasa ikiwa tumo katika kumi la Rehma.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atupe nguvu na ustahamilivu, na atuwezeshe kufunga Mwezi wote . Vilevile, tunamuomba azipokee funga zetu, azikubali dua , sala na ibada zetu zote , na atuwezeshe kumuabudu zaidi siku zote pamoja na kuudiriki Usiku mtukufu wa laylatul-Kadri. Pia tunamuomba Mwenyezimungu atujaalie kutenda mema kwa mwezi mengine yote inayofuata.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya chombo hiki muhimu cha wananchi, ili kuweza kutoa maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Habari , Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka wa fedha 2018/ 2019.

Pia, nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Baraza kwa kuliongoza Baraza hili tukufu, naamini kwamba mtaliongoza Baraza hili kwa uadilifu wa hali ya juu na kuimarisha Demokrasia katika muhimili huu muhimu wa dola katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inachukua nafasi hii, kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein pamoja na wasaidizi wake wote kwa kuiongoza vyema nchi yetu, huku wakitekeleza kwa vitendo Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi. Bila shaka wananchi wetu wataendelea kukiunga mkono Chama cha Mapinduzi kutokana na kutekelezeka vyema kwa ilani yake.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inaunga mkono mabadiliko yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais wa Zaiznabr katika Wizara hii kwa kuongeza baadhi ya taasisi na nyengine kuzipeleka sehemu nyengine, tukiamini kuwa hatua hii itaongeza ufanisi wa utendaji ndani ya Wizara na taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, Kipekee kwa niaba ya Kamati, nimponngeze sana Mwakilishi wa Jimbo la Welezo Mhe. Hassan Khamis Khafidh (Diaspora), *Mwakilishi wa Wakwezi na Wakulima* ambae alikua Mjumbe wa Kamati hii, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda. Kamati inaamini kwamba uteuzi wa Mheshimiwa Diaspora Kuwa Naibu Waziri umekuja katika wakati unaofaa. Tunaamini kwamba kutokana na uzoefu alioupata katika Kamati hii hivi sasa atakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kuwatetea wajasiria mali wetu na wanaushirika kwa ujumla, katika kuwatafutia viwanda vidogo vidogo vya usarifu wa mazao na kuwatafutia masoko ya uhakika na hatimae kufanikiwa katika shughuli zao za uzalishaji hadi hatua nzuri zaidi yaani ***From Zero to Hero!***

Mheshimiwa Spika, Sina budi pia kumshukuru Waziri wa Habari, Utalii, na Mambo ya Kale, Naibu wake Mheshimiwa Choum Khamis pamoja na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kupitia makadirio ya Bajeti ya Wizara hii. Lakini pia nawashukuru Wajumbe wa Kamati yetu kwa umoja wao na kazi nzuri waliyoifanya kiasi cha kunirahisishia kazi yangu ya kuongoza kikao kuwa nyepesi zaidi, kwa hakika wameweza kuijadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoidhinisha zinatumiwa kwa matumizi yaliokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kwa heshima ya hali ya juu napenda kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama hivi ifuatavyo:-

1.	Mheshimiwa Ali Suleiman Ali (SHIHATA)	Mwenyekiti
2.	Mheshimiwa Salha Mohammed Mwinjuma	Makamu Mwenyekiti
3.	Mheshimiwa Maryam Thani Juma	Mjumbe
4.	Mheshimiwa Zaina Abdalla Salum	Mjumbe
5.	Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub	Mjumbe
6.	Mheshimiwa Mussa Foum Mussa	Mjumbe
7.	Ndugu Himid Haji Choko	Katibu
8.	Ndugu Mussa Issa Mussa	Katibu
9.	Ndugu Amina Abeid Hemedi	Mkalimani

Mheshimiwa Spika, Pongezi zaidi zimwendee Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub , Mwakilishi wa Jimbo la Paje na Mjumbe wa Kamati hii ambae pamoja na kwamba ni Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, amekuwa akijitahidi sana kushiriki kikamilifu katika kazi za Kamati yetu bila ya kuathiri majukumu yake huko Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Kabla sijaingia katika Bajeti ya Wizara napenda pia Kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti , Mheshimiwa Mohammed Said Mohammed (Dimwa) pamoja na watendaji wa Wizara ya Fedha ambao walitoa miongozo na mchango mkubwa wakati wa kupitia bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Baada ya utangulizi huo sasa naomba nitekeleze jukumu lililonileta hapa mbele ya Baraza lako tukufu ambapo, Kamati yangu inapongeza Juhudi zilizochukuliwa na Wizara hadi kukusanya asilimia **110**, kwa taasisi zilizoruhusiwa kutumia na tunazihimiza taasisi zilizomo katika Wizara hii, ambazo zinazoingiza mapato yake moja kwa moja katika Hazina, na hazikuweza kufikia malengo, nazo ziongeza bidii ya ukusanyaji, ili kufikia lengo lililokusudiwa. Kamati inaitaka Wizara kuibua zaidi vianzio vipya vya mapato na hatimae kuongeza mapato ya serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi tunazozitoa kwa taasisi zote zinazohusika na utekelezaji wa program ya Maendeleo ya Habari na Utangazaji na Upigaji Chapa. ambavyo ni vyombo vyote vya Utangazaji vya Serikali, bado Kamati yangu hairidhishwi na tabia ucherewaji wa utoaji taarifa kwa taasisi hizo. Kwa kweli utowaji wa habari kwa taasisi hizi hauendi sambamba na wakati wa sasa wa ukuwaji wa kasi ya maendeleo ya sayansi na Technolojia ya habari .

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa mfano wa tukio la utiaji wa Saini makubaliano ya Ukarabati wa jengo la Beit-el-Jaib hivi karibuni baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Oman , tukio ambalo Mwenyekiti wa Kamati hii alilishuhudia. **Mheshimiwa Spika**, ilichukua takriban dakika tano (5) tu, baada ya kusainiwa Mkataba huo habari hizo zilienea ulimwengu mzima kupitia mitandao ya kijamii na vyombo vyengine vya habari , lakini kwa mshangao mkubwa Habari hiyo hiyo ilichukua karibu siku mbili, ndio baadae ikatangazwa na Shirika letu la Utangazaji la Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Mifano ya haya iko mingi sana hapa Zanzibar, kumekuwa na matukio mengi katika jamii yetu na ulimwenguni kwa ujumla, lakini vyombo vyetu vya habari vya Umma vimekuwa vikicherewa sana kuyatangaza ukilinganisha na vyombo vya watu binafsi. Kamati inahimiza kurekebishwa kwa hali hiyo na kujenga tabia ya kutoa habari mapema na kwa haraka, au angalau kutoa kwa muhtasari tu habari za matukio hayo, na baadae yakishayafanyia utafiti wa kina yatangazwe kwa ukamilifu wake.

Aidha, Kamati pia inashauri Taasisi za habari za umma kuzungumza na Makampuni ya simu, ili waweze kuyatumia kutangaza habari za papo kwa papo kwa Muhtasari kupitia njia ya ujumbe mfupi kila yanapotokea kama zinavyofanya taasisi nyengine.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu bado inawasiwasi wa Umiliki na Uendeshaji wa Channel ya ZBC TWO (2). Tumearifiwa kwamba , Shirika la Utangazaji la Zanzibar ZBC limefunga mkataba na Kampuni ya Azam Media LTD miaka kadhaa iliyopita kwa ajili ya uendeshaji wa Channel hiyo, ingawa Kamati hadi inapitia Bajeti ya Wizara hii haikuoneshwa Mapato yanayotokana na matangazo ya ZBC 2.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kwamba ZBC bado ndio Mdomo Mkuu wa Serikali, na wananchi waliowengi zaidi licha ya ongezeko kubwa la vyombo vya utangazaji hapa nchini, bado wanalipenda na kuliamini Shirika lao la Utangazaji, hivyo wakati tunaingia mikataba na watu binafsi kuendesha ZBC 2, Kamati inaishauri Wizara kuwa makini zaidi na suala hili, na pia tunashauri mkataba huu upitiwe upya na uwe wazi, huku tukiangalia maslahi mapana zaidi kwa serikali na wananchi wake na kwa wakati wa sasa na wakati ujao.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake , Habari na Utalii pia inashauri ZBC kuwa na rekodi nzuri ya mikataba baina yake na taasisi zote zinazotumia minara yake ya Masingini, Dole , Bungi, Kichunjuu na mingineyo kwa kuweka vifaa vyao vya mawasiliano ama matumizi mengine na kuhakikisha kwamba taasisi hizo zinalipia huduma zao na kuongeza Mapato kwa shirika.

Kamati inashauri zoezi hilo liende sambamba pamoja na kudai gawio kwa Makampuni ya Simu ambayo *line* zake zinatumiwa na wasikilizaji ama watazamaji wakati wa vipinndi vinavyotumia simu katika vipindi vya moja kwa moja yaani *live* ,vinavyorushwa na Shirika hili.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhika na kazi zinazofanya na kituo cha ZBC Dar- es-Salaam ikiwemo utumaji wa wastani wa Habari (*Story*) mbili kwa siku pamoja na kuandaa Kipindi cha Dondoo za Magazetini, Jarida la Wiki na Rege Pawa (*Reggae Power*). Kamati inaiomba Wizara kuzidi kukiimarisha kituo hiki kwa kukipatia rasilimali watu na vifaa. ZBC kituo cha Dar-es-Salaam kama kitatumiwa vizuri kinaweza kutumika kama ni chanzo chengine cha mapato kupitia matangazo ya wadhamini wa

kipindi cha dondoo za magazetini ambacho hivi sasa kimejipatia umaarufu mkubwa kwa wasikilizaji wa ZBC Redio.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza hatua ya Idara ya Habari Maelezo ya kufunga Ubao wa matangazo ya kielektroniki (*Electronic Display Board*) katika eneo la Mnara wa kumbukumbu ya Mapinduzi Michezani. Hata hivyo, Kamati inashauri huduma hiyo ikaimarishwa zaidi na hatimae ilete mvuto mkubwa kwa wananchi na taasisi mbali mbali ambazo zinaweza kushawishika kutoa matangazo kupitia ubao huo. Aidha, Kamati inahimiza mibao kama hiyo iendelee kuwekwa katika sehemu mbali mbali zenye mkusanyiko mkubwa wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefurahishwa na uwamuzi wa Serikali wa Kuamua Gazeti lake la Zanzibar leo kuchapishwa hapa Zanzibar, hatua ambayo imeharakisha upatikanaji wa gazeti hilo mapema zaidi hapa Zanzibar. Hata hivyo, Kamati yangu bado inalishauri Shirika la Magazeti la Zanzibar kufikiria namna bora zaidi, ili kuhakikisha Gazeti lake linafika katika soko la Mikoa ya Tanzania Bara kwa wakati na sio kiporo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inasikitishwa sana na tabia ya baadhi ya taasisi za serikali ambazo zinakataa kuchukuwa Gazeti la Zanzibar leo ambalo huwa limesheheni taarifa nyingi za maendeleo ya nchi zinazofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, Kamati haitoacha kutoa kilio chake kwa taasisi ambazo zinapata huduma ya matangazo kupitia gazeti hili na baadae kushindwa kulipia matangazo hayo. Kwa kweli, madeni haya yanawarudisha nyuma watendaji wa gazeti hilo, na Kamati inatoa wito kwa taasisi hizo kusawazisha madeni yao, ili kuliongezea mapato na kuongeza ari ya utendaji katika gazeti hilo.

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Mheshimiwa waziri inaonesha kwamba Tume ya utangazaji Zanzibar inaendelea kupokea na kupitisha maombi ya leseni za utangazaji hapa Zanzibar. Kamati inapongeza hatu hiyo, huku ikipongeza ukuaji na maendeleo ya Sekta hiyo. Kamati inahimiza ukuaji huo wa sekta ya Utangazaji, hauna budi kwenda sambamba na Sheria na Maadili ya Utangazaji .

Sambamba na hilo, Kamati inapongeza ongezeko la Online TV na Redio pamoja na Mitandao ya Kijamii lakini inashauri kwamba, kuwe na udhibiti maalum kwa kuvitambua vyombo hivyo na wamiliki wake pamoja na kuviwekea miongozo maalum, ili kuhakikisha kwamba havikiuki maadili, Silka na Utamaduni wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyengine tena, Kamati yangu inaiomba Wizara kuvitambua na kuvithamini nyombo vya habari vya watu binafsi kutokana na mchango wao mkubwa katika sekta ya habari na maendeleo hapa nchini, angalau kukaa nao kila baada ya Muda na kujua Mafanikio na changamoto zinazowakabili.

Mheshimiwa Spika, Baraza hili ni shuhuda wa hayo kwani hotuba mbali mbali za mawaziri wanaokuja mbele yako, zinaonesha kwamba, pamoja na vyombo vya Serikali pia huvitumia sana vyombo vya watu binafsi kutoa taaluma mbalimbali zinazohusiana na taasisi zao.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imeridhika na Shabaha za Mwaka huu za Wakala wa Uchapaji Zanzibar, ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa zaidi. Tunaziomba taasisi zote za serikali na watu binasfi kukitumia Kiwanda cha Uchapaji kwa shughuli zote zinazohusiana na machapisho ya aina zote. Aidha, tunaomba Kiwanda kijitahidi kujitangaza ndani na Nnje ya Zanzibar ili, jamii izidi kufahamu huduma zinazopatikana kiwandani hapo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaliomba Baraza lako tukufu kukubaliana na maoni ya Kamati kwa kukubali fedha zote zilizoombwa kwa ajili ya kutekeleza Programu Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Utunzaji wa Nyaraka na

Kumbukumbu inayolenga kuwa na maeneo ya kihistoria yaliyoimarika na kuwepo na usimamizi imara wa Kumbukumbu na Nyaraka.

Mheshimwa Spika, Kamati inasisitiza uaminifu wa hali ya juu katika matumizi ya fedha zinazotengwa kwa ajili ya uendelezaji wa maeneo ya kihistoria na magofu. Kwa kweli, magofu mengi hivi sasa hayako katika hali nzuri ingawa fedha zinazoombwa kwa ajili ya uhuishaji wa sehemu hizo zimekuwa zikipatikana lakini maendeleo yake huwa hayaonekani na kupelekea historia kubwa katika baadhi ya maeneo hayo kuanza kupotea.

Aidha Kamati inashauri kufanyiwa matengenezo Gofu moja baada ya jengine badala ya kuyafanyia yote kwa wakati mmoja na hatimae kutoonekaana kinachofanyika. Kamati, inamshauri Mheshimiwa Waziri kuwa karibu zaidi kufuatilia matumizi ya fedha zinazotengwa kwa ajili ya Kuendeleza sehemu za Magofu na za Kihistoria.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaendelea kusisitiza haja ya kuwekwa au kufanyiwa matengenezo vyoo katika sehemu zote za magofu na sehemu nyengine za kihistoria, ili kutunza mazingira katika sehemu hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati itakuwa haijaitendea haki Programu hii ikiwa haijatoa pongezi zake kwa Serikali baada kufunga Mkataba na serikali ya Oman unaohusu kulifanyia matengenezo jengo la Beit-El-Ajaib ambalo ndio roho ya Historian ya makumbusho ya Mji Mkongokwe na Zanzibar Kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhika na maelezo ya jumla kuhusiana na kupatiwa ufumbuzi tatizo la ukosefu wa Ofisi ya Nyaraka Pemba baada ya kufanyiwa matengenezo makubwa Jengo la Mahakama ya Kale Kichungwani Pemba, na kuanza kutumika kuanzia Mwezi Januari mwaka huu. Aidha Kamati inachukua fursa hii kuwasisitiza wafanyakazi wa Nyaraka Unguja na Pemba kuwa waaminifu na kudhibiti siri za Serikali na hatimae kupata usalama wa Nyaraka zetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeripoti kupatiwa ufumbuzi changamoto ya muda mrefu ya kukosekana kwa takwimu sahihi za utalii kwa kuondosha kasoro zilizokuwepo katika mfumo wa upatikanaji wa takwimu hizo. Kamati inatoa pongezi za dhati kwa hatua hiyo na inashauri kuharakishwa kwa mfumo wa kisasa wa kielektroniki, ambao utafuatilia mwenendo mzima wa mgeni kwa kipindi chote atakachokuwepo nchini. Hata hivyo, Kamati inazidi kushauri kwamba, hatua hii ya uboreshaji wa upatikanaji wa takwimu sahihi za utalii, lazima iende sambamba na mapato halisi yanayotokana na sekta hii kulingana na takwimu hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaridhishwa na juhudi zinazochukuliwa na Wizara kwa kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanashiriki kikamilifu katika shughuli za kitalii, tunashauri elimu ya utalii izidi kutolewa katika Skuli za Msingi na Sekondari nchini kote, wananchi wazidi kushajihishwa kutembelea na kuvitunza vianzio vya utalii. Aidha, tunaiomba Serikali iingize mkono wake kidogo katika matamasha mbali mbali kama vile Sauti ya Busara, ZIFF, Rafiki Network , Tamasha la Vyakula vya Asili na Mwakakogwa Makunduchi na mengineyo ambayo tunaamini yanasaidia kwa kiasi kikubwa kutangaza Utalii ,Utamaduni , Uchumi wa Taifa na ajira kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu bado inasikitishwa na jinsi tunavyowakaribisha wageni hapa nchini kupitia uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume Kisauni, kwa kweli wakati tunasubiri kukamilika kwa jengo Jipya la Abiria la Terminal II (two), tunashauri kufanyika kwa ukarabati wa dharura, ili kuhami sehemu ya wanaowasili yaani ***Arivals*** katika uwanja huo.

Mheshimiwa Spika , kuna taarifa kadhaa zisizoridhisha juu ya kadh-ya inayowapata wageni ambayo ni hatari kiusalama kwa afya zao, hasa siku za msimu ambapo hupelekea wageni wengi kwa wakati mmoja. Hali ya Joto kali na ufinyu wa nafasi katika sehemu hiyo , nayo inachangia kwa kiasi kikubwa kutoa sura mbaya kwa wageni wetu.

Mheshimiwa Spika, Aidha Kamati yangu pia inashauri kupitiwa upya miongozo ya watembezaji watalii yaani **Tour Guard** , ili kuwatambua na kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa uzalendo na uwaminifu mkubwa bila ya kupotosha Historia ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza juhudi za Wizara za kuimarisha mazingira ya kazi Ofisi Kuu Pemba, ambapo Wizara imeripoti kuzipatia taasisi zilizopo chini yake nyenzo na vitendea kazi. Hata hivyo, Kamati bado inasisitiza haja ya kupatiwa ufumbuzi tatizo la ufinyu wa nafasi kwa taasisi hizo ambazo bado zinaendelea kubanana katika jengo la afisi hiyo Chakechake Pemba.

Mheshimiwa Spika, bado Kamati inahimiza kuharakishwa tafiti zote, mapitio ya Sera na Sheria zinazoongoza Wizara ili iweze kutekeleza majukumu na mipango yake kwa ufanisi unaohitajika.

Mheshimiwa Spika, Kabla sijamalizia hotuba yangu, napenda sasa kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu mkubwa, pia napenda kukushukuru kwa mara nyengine tena wewe binafsi kwa kuniruhusu kutoa maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kuhusiana na Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Baada ya maelezo hayo, napenda kutamka kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake Habari na Utalii na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kijito Upele, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale . Aidha nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote waijadili, wachangie na hatimae waunge mkono Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii kwa kuidhinisha shilingi **16,491,400,000/=** kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu na malengo waliyojipangia**.**

Mheshimiwa Spika, Naunga mkono hoja.

Ahsante,

……..

Mhe. Ali Suleiman Ali (**SHIHATA**),

Mwenyekiti,

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii,

Baraza la Wawakilishi,

Zanzibar.